# NAMNA LUGHA YA KISWAHILI ILIVYOINGILIANA NA DINI YA KIISLAMU, AFRIKA MASHARIKI.

NA AHMED SHEIKH NABHANY

UISLAMU ulipoingia Afrika ya Mashariki katika karne ya saba A.D. Waswahili waliupiga pambaja na kutoka siku ile lugha ya Kiswahili pamoja na tungo zake zikaathiriwa sana na Uislamu na lugha ya Kiarabu.

Lugha ya Kiswahili ikakopa maneno mengi muhimu kutoka Kiarabu. Kukopwa huko kwa maneno haya hakumaanishi kuwa Kiswahili kilikuwa na upungufu wa maneno ya kuelezea mawazo fulani fulani. Kiswahili ni lugha inayojitosheleza lakini kwa sababu ya mapenzi ya dini na kwa sababu mawazo fulani ya dini yaeleweka kwa urahisi zaidi kwa kutumia maneno ya Kiarabu. Waswahili wakawa wakitumia maneno ya Kiarabu na kuyaingiza katika lugha ya Kiswahili. Athari hii ikatajirisha msamiati wa Kiswahili.

## KUBUNI IRABU

Athari nyiingine ni kuwa wataalamu wa Kiswahili wakabuni maandishi yao kwa kutumia herufi za alfabeti za Kiarabu. Waligundua kuwa katika Kiarabu hakuna irabu za E na O na pia silabi kama cha, pa, va, nga, nja na kadhalika. Kwa hivyo, wakabuni irabu hizo ili Kiswahili kiweze kuandikika kikamilifu.

Walipoipata ala hii ya kuandikia, washairi wa Kiswahili wakawa wakitunga bahari mbali mbali za mashairi juu ya mambo ya dini na ya kidunia. Moja katika maandishi ya kwanza ilikuwa ni utungo wa "Hamziya" au "Ummul Qura".

Utungo huu ulikuwa ni tafsiri ya Aidarus bin Athman bin Ali wa mwaka wa 1749 kwa Kingozi, yaani Kiswahili cha kale. Ulitafsiriwa kutoka shairi la Kiarabu lililotungwa zamani na Shekh Muhammad bin Said Albusiry wa Misri.

Utungo mwingine maarufu ni wa Sayyid Abdalla bin Ali Nassir wa Pate uitwao "Inkishafi". Utungo huu ni maarufu sana katika ulimwengu wa Kiswahili. Mshairi hapa anaeleza jinsi ustaarabu wa mji wa kale wa Pate ulivyofikia kilele cha ufanisi na halafu ukapotea na ukawa ni funzo kwa mwanadamu.

Tungo nyingine zenye maudhui ya dini zilizotungwa zamani ni "Waji Waji" na Dura-Mandhuma". "Waji Waji" ulitungwa na Sayyid Omar bin Amin wa Lamu na "Dura-Mandhuma" na Sayyid Mansab bin Abdulrahman. Utungo wa "Dura-Mandhuma" uliandikwa kwa ufundi mkubwa. Ukieleza mambo ya dini na ya maadili, umetungwa kwa kufuata herufi za alfabeti za Kiarabu kwa kutegemea irabu tatu maarufu za Kiarabu za A, I na U. Waislamu hupenda kuuimba utungo huu kwa njia ya kasida.

Maelezo ya athari ya dini ya Kiislamu katika Kiswahili hayawezi kukamilika bila kutaja utungo wa "Utenzi wa Tabuka" (au "Utenzi wa Herekali") Utenzi huu ulitungwa mwaka wa 1728 na Mwengo bin Athman wa Pate kueleza vita vilivyopiganwa baina ya jeshi la Waislamu lililoongozwa na Mtume Muhammad (S.A.W.) na jeshi la Warumi lililoongozwa na Gavana Herecleos katika mji wa Tabuk kaskazini ya Arabuni. Ndio maana utungo huu wajulikana kama wa Tabuka au Herkali.

## WASHAIRI MASHUHURI

Kwa vile tungo za Kiswahili zilizoathiriwa na Uislamu si lazima zieleze habari za dini tu, walikuwako washairi fulani waliotunga juu ya mambo ya maadili kama vile nasaha. Kwa mfano, mshairi mmoja maarufu sana alikuwa ni mwanamke aliyeitwa Mwana Kupona binti Mshamu. Aliishi katika mji wa Pate. Katika mwaka wa 1858 alimtungia binti yake Mwana Hashima binti Sheikh Mataka "Utenzi wa Mwana Kupona" kumwusia jinsi ya kuishi vizuri na mumewe na kwa jumla jinsi mwanamke anavyopaswa kuishi kwa kufuata maamrisho ya dini.

Utenzi huu ni mmoja katika tungo maarufu za Kiswahili. Wasichana wengi wa Kiislamu walikuwa wakifunzwa kuuhifadhi ili uwe ni mwongozo mzuri katika maisha yao.



**HILI NI kundi la waalimu wa msingi kutoka Kwale baada ya kumaliza waksha yao juu ya elimu ya dini katika misheni ya Samburu mwaka huu.**
PICHA: COURTESY "READ"



*BANDI MARIDADI kutoka Bamburi Portland Cement ambayo iliwatumbuiza wananchi wengi waliohudhuria tamasha za siku ya elimu ya gumbara katika kituo cha shule ya Msingi ya Mlaleo.*
PICHA: CEASAR MADDANGANHA

# Pongezi kwa Rais Moi, kwa kuwatetea Madereva

RAIS WA Chama kinachotawala cha KANU, na Rais wa Taifa la Kenya Muheshimiwa Daniel Arap Moi, Ijumaa iliyopita huko Wilaya ya Kiambuu, alitoa mawaidha ya busara sana ambayo yanastahiki kuzingatiwa na kutekelezwa na kila mmoja wetu iwapo tunapenda amani na umoja udumu katika Taifa letu la Kenya. Rais Moi akihutubia umati mkubwa wa wakaazi wa Kiambuu na vitongoji vyake, aliwashutumu vikali maafisa ambao hudharau uanadamu wa madereva wao kwa kufanya dharau ya kuwakumbuka wakati wa kuendelea na starehe zao.

Rais Moi alishangazwa na kuona afisa, anatoka kwenye gari kuanzia saa za jioni akaingia kwenye baa hadi saa nne za usiku na wakati wote huo huyo dereva maskini yumo ndani ya gari anamsubiri bosi wake amrudishe nyumbani. Rais akiwa na hamasa, alisema kwamba hawa madereva, ni wanadamu. Wao wana mabibi nyumbani na baadhi yao pia wako na watoto. Mara madereva wamalizapo kazi yao, kama mfanyikazi yoyote hupenda kurudi nyumbani kama mzazi ili kuangalia hali ya watoto wake na kujumuika nao kwa wakati uliobakia. Na Rais akaonya kwamba kama mfanyikazi yoyote, dereva lazima afanye kazi kwa masaa yale yale anayofanya kazi mfanyikazi mwengine yeyote. Yaani masaa ya kazi yakimalizika basi dereva naye yuko huru kwenda kuangalia shughuli zake nyengine.

Maafisa wenye vyeo vikubwa na daraja kubwa katika kazi zao, ni budi waitikie mwito huu wa Rais na bila ya kufikiria kwamba hadhi zao zimepunguzwa iwapo madereva hawatawapeleka kwenye shughuli zao zisizokuwa za kikazi. Ukweli ni kwamba maafisa ambao kwa heshima ya kazi zao hubidi kupatiwa gari la serikali, petroli ya serikali na dereva wa serikali, kwa ajili ya kuhudumia Taifa wengekuwa na shukurani za kutosah kwa serikali na raia wote kwa ujumla kwa heshima hiyo aliyopawa. Fedha za kunua gari hilo, na za kununulia petroli ya kuendesha gari hilo na fedha ya kulipa mshahara wa kuendesha gari hilo zatoka katika mfuko wa kodi. Raia ambaye hulipa kodi hiyo, yeye binafsi huenda kazini kwa basi, matatu na katikati ya mwezi kwa maguu.

Hata hivyo zingatio kubwa zaidi katika mawaidha ya Mtukufu Rais, mbali na kumtumisha dereva masaa baada ya kazi, hakuna haja ya kumfanya kibarua kuwa yeye ni mtu duni kwa ajili ya kazi yake anayoifanya, maana kazi zote mbele ya macho ya serikali zina umuhimu wake katika maisha ya wanadamu na ndipo serikali ikalipa mshahara wa kila kibarua na pia kumlinda katika kazi yake.

Yaani vyeo vyetu visiwe ni leseni ya kukejeli wenzetu ambao hawana elimu kama zetu. Kazi ya kila mtu ni muhimu na kila mmoja anahitajia huduma kutoka kwa mwengine ndipo maisha yake yaweze kumwendea. Bila ya shaka funzo la Rais litazingatiwa kikamilifu kwa madhumuni ya kudumisha upendo na umoja. Kwa vile ni wazi kwamba Rais Moi ampenda kila raia wa nchi hii awe tajiri ama masikini, ni wazi kuwa iwapo hatua ya kulinda magari ya serikali yatumika kwa wakati wa kazi pekee, atahakikisha kwamba madereva wa serikali wanazingatiwa kama mfanyikazi mwengine.

# Dini ya Kiislamu imesimama juu ya Haki

**NINACHUKUWA NAFASI hii kumpongeza Bwana Burhan kwa makala yake marefu yaliyotokea katika toleo la CW 20-26/8/82. Hakika Bwana huyu ametudhihirishia ujasiri wake, na utafiti wake wenye kuridhisha kwa yeyote mpenda haki na usawa. Watu kama yeye wanahitajika sana katika duniya hii yakileo. Hakika wale ambao kwahakika wamehusika na njama kama hizo, ningaliwaomba waepukane na majambo kama haya kwamanufaa yao wenyewe yahapa duniani nakesho akhera. Wanakhiyari yakujirekibisha ama la.**

**Hapo hapo ninachukuwa nafasi hii kumtahadharisha Bwana A. A. Mohamed, Lamu kwa baruwa yake iliyotoka katika toleo la CW 27/8-3/9/82. Hakika imetudhihirikia wazi, na tunashauku kubwa yakuwa huenda ikawa labda ana damu yahao mawalii waliotajika katika makala ya Bwana Burhan. Hakika ameshindwa kutubainishia ni Aya gani haswa inayosisitiza yakuwa Sadaka ama Zawadi zinazotoka nchi zanje kwamadhumuni ya kuwasaidia, ama kwamanufaa ya waislamu wote, ipeanwe kwa watu fulani, waukoo fulani, ama misikiti fulani. Ama niwapi katika Quran tukufu panaposema yakuwa kabila fulani katika waislamu nibora kuliko kabila fulani? Ninavyofahamu mimi hiyo sadaka inayomlazimu mtoaji kwanza kuwakumbuka jamaa zake wakaribu, niyayule mtoaji binafsi sio hiyo inayotoka mbali kwaajili yawatu wote halafu igawanyiwe vipote fulani. Hizi sizo siku zile zakuambiwa niharamu kufasiri Quraan, siku zile zimekwisha haki sasa imezagaa, na Ishallah ubatilifu utatoweka AMIN.**

**Vile vile ningalipenda kumtanabahisha yakuwa, silazima kwa Bwana Burhan kufuata njia kama hiyo iliyoko sasa yakujinufaisha binafsi kwakuomba misaada kama hiyo kutoka nchi za nje, ama kutoka kwa Sheikh Abdalla kama alivyodai. Kuja kwa misaada kama hiyo hakuna manufaa yeyote isipokuwa kunufaisha watu fulani fulani kama inavyodaiwa.**

**Vile vile silazima, wala haitakuwa ni sifa yakulazimika Bwana Burhan naye amuombe Sheikh Abdalla huko aliko naye atume zawadi ama sadaka kama hizo. Hakika wengi wetu sio Kenya tu, karibu Bara la Mashariki nzima tumenufaika, ilimika, na kuerevuka kutokana na masomo tuliyopata kwa Sheikh Abdalla. Hiyo pekeyake ni sadaka tosha ambayo imegawanyika karibu bara zima la mashariki ya Afrika, licha yahizo sadaka zinakuja Mombasa pekeyake.**


**Ninamuomba anieleze ninani katika masheikh wetu waliowahi kuzagaza sadaka kama hii, inafaida gani iwapo sadaka itakayotufaa kesho akhera ikiwa tunayo kuomba anasa zaduniani, ambayo ikifika hapa huwa ni Yariya na Mapendeleo ambayo wengi wetu tunaizingatia kwa Nihabaan Manthura.**

*Ishak Y. M. Mtambua.*
*MOMBASA*

# JISHINDIE

## *MIAVULI AU T-SHIRT MARIDADI KATIKA SHINDANO JIPYA LA KUJAZA MANENO.*

## SWAHILI CROSSWORD NO 147



*KWENDA KULIA:*

1. Mala ni mlaleo mla jano
5. Wingi wa yeye
6. Cha moto
7. Kulalia kwa kuku juu ya mayai
9. Ama
10. Chombo cha bahari
12. Watetea ... mgomba si wao
14. Aina ya ndege
15. Kiungo cha maneno
16. Zidisha

*KWEDA CHINI:*

1. ... kinguoni mwako
2. Shabaha
3. Mwenda tezi na omo maregeo ...
4. Huvaliwa shingoni
5. Hunukia linapochanua
8. Tamko la kukataa
11. Mwenziwe mshale
12. Ufupi wa "Na wao"
13. Jitu zima
15. West Africa

**Washindi wa Fumbo la Kujaza Maneno No. 145**

1. Faschal Chagembe, Sanduku La Posta 84968, Mombasa
2. Abudi Bwanaidi, Sanduku La Posta Mwikaa Mtenzi 81543 MOMBASA.
3. Abbasi Shaffi Sanduku la Posta 87922, Mombasa

**Washindi waombwa wafike afisini mwa *COASTWEEK*.**

**MAJIBU YA SHINDANO LA FUMBO LA KUJAZA MANENO NO. 146 —**

*KWENDA KULIA:*
1. MWAVULI, 6. NENEA, 8. IRINGA, 9. TEO, 10. MKAUMA 13. TAMBAA, 16. JE, 17. UA, 18. KIZIMBA.

*KWENDA CHINI:*
2. WARAKA, 3. UNGAMA, 4. LEA, 5. IN, 7. ELEKA, 11. UTESI, 12. AMALI, 14. AULA, 15. ZUA.

JINA ..............................................

SANDUKU LA POSTA ..............................................

..............................................

**Shindano la Fumbo la Kujaza Maneno:-**

Uamuzi wa majaji utakuwa wa mwisho. Hakuna malalamiko yoyote yatakayokubaliwa. Washindi watatu kila baada yawiki mbili watapata miavuli au T-shirt maridadi. Shindano hili limeshaminiwa na *COASTWEEK* Limited Mombasa.
Jawabu za Fumbo hili lipekelwe kwa Muhariri *COASTWEEK* Sanduku La Posta 87270, Mombasa Kenya.
Siku ya Jumatano tarehe September 22, 1982 saa nne asubuhi shindano hili litakuwa mwisho.